# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAM TANZANIA <TAHISCO>

## MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

## KIDATO CHA SITA

## KISWAHILI - 2

## MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

# MWONGOZO WA USAHIHISHAJI
# KIDATO CHA SITA
# KISWAHILI - 2

## SEHEMU A: (ALama 40)

Mtahiniwa anatakiwa ajibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Swali linamtaka mtahiniwa kuonesha uwiano wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi simulizi ili kujenga au kupata kazi bora.

(i) Hutumia Wahusika kufikisha ujumbe
(ii) Hutumia Mtindo kuibua au kufikisha dhamira mbalimbali
(iii) Hutumia mandhari kuibua au kufikisha ujumbe na dhamira
(iv) Hutumia muundo kuibua au kufikisha dhamira
(v) Hutumia matumizi ya lugha kuibua ujumbe, dhamira na migogoro.
(vi) Hutumia Wahusika kuibua migogoro.

Zingatia: mtahiniwa akitaja kipengele chochote cha fani chenye mahusiano au uwiano na maudhui apewe alama.

(Alama 02 @ 10)

2. Swali linamtaka mtahiniwa aeleze vipera vitano vya hadithi ambavyo ni:-

(i) Ngano
(ii) Tarihi
(iii) Visasili
(iv) Vigano
(v) Soga
(vi) Hekaya

(Alama 02 @ 10)

3 Swali linamtaka mtahiniwa kueleza vikwazo vitano (5) vinavyoingilia uhuru wa mtunzi wa kazi ya fasihi.

(i) Kuwepo katika mfumo fulani usio mzuri
(ii) Kuwepo kwa udhamini wa nguvu
- Baadhi ya watunzi hulazimishwa katika utunzi au kudhamini wa jambo ambalo huathiri suala la utunzi.
(iii) Uoga na kutojiamini / ukosefu wa utashi.
- Hii humpelekea kutokuwa huru katika utunzi wa kazi za fasihi
(iv) Msukumo kutoka tabaka tawala au kukosekana demokrasia.
- Hufungia kazi za fasihi pale linapoona limesemwa
(v) Kutokuwepo na uwezo wa kuitawala lugha yake au Sanaa yake.
(vi) Umaskini / ukosefu wa pesa
- Baadhi ya watunzi, umaskini hupelekea kushindwa kutunga kazi bora

Zingatia: Na nyinginezo.
(Alama 02 @ 10)

04 Swali linamtaka mtahiniwa abainishe mbinu za kifani zilizotumika katika matini husika.

I. Muundo Msago au Moja kwa moja
Mtunzi ametumia muundo wa moja kwa moja. Kwa kusimulia matukio mbalimbali kama vile Sikitu alipokuwa analalamika kuharibikiwa kwa Chuku na Chipepe kupigwa na Sikitu.

II. Mtindo.
- Mtindo wa dayolojia (majibizano).
mfano. Mazungumzo ya chuku, Sikitu, mama chuku na chipepe

- Mtindo wa matumizi ya nafsi,
mfano: Nafsi ya tatu Umoja: Chuku (anaanza kulia)

III. Wahusika
- Chuku, mtoto wa Mama chuku
- Chipepe, Sikitu.

IV. Mandhari / Muktadha.
- Mandhari ya nyumbani: mfano: Nyumbani kwa Mama chuku na Baba chuku. (Mandhari hii yote ni mandhari halisi)

V. Matumizi ya Lugha.
- Matumizi ya Nidaa. Mfano- Eeh! ukweli unauma sasa--
- Matumizi ya mdokezo mfano. Ukweli unauma sasa....
- Matumizi ya takriri: mfano: Sikitu: (Chuku akicheka): Eeh!.. Eeh!... Eeh! na Unaonesha kuwa ni mkali Sana! sana! Sana
- Onamatopea (Tanakali sauti) mfano- ochchchchch
(Alama 2 @ 10)

SEHEMU B: (Alama 60)

Mtahiniwa anatakiwa kujibu maswali matatu (3) tu katika sehemu hii. Swali la saba ni la lazima.

5. Swali linamtaka mtahiniwa kuonesha namna watunzi wa kazi za fasihi wanavyochochea kuleta mabadiliko chanya kwa jamii za kiafrika.

FUNGATIE YA UHURU
1. Kupiga vita uongozi mbaya: Shairi La HAKI, VIONGOZI WA AFRIKA, NJAMA N.K.

5

II. Kukemea suala la usaliti: Katika shairi la TUMESALITIWA, FUNGATE n.k

III. Kupiga vita suala la Dhulma: Shairi la WIZI

IV. Kupiga vita Unyonyaji: Shairi La NAONA

V. Kukemea matabaka: Shairi la WAJA WA MUNGU, FUNGATE. n.k.

## CHUNGU TAMU

I. Kupiga vita usaliti katika jamii: Shairi la CHUNGU TAMU, CHATU NA KUKU, n.k.

II. Kupiga vita Uongozi mbaya katika jamii shairi: CHUNGU TAMU, TISHIO LA BINADAMU, CHANZO NI WENYE KAULI n.k

III. Kuhamasisha jamii kukua na uzalendo: shairi la DAKTARI ASKARI,

IV. Kupiga vita matabaka: Shairi CHATU NA KUKU, MANZESE MPAKA OSTABEI, THOMAS NA DOTTO n.k.

V. Kuhamasisha mapenzi ya kweli: Shairi La THOMAS NA DOTTO.

## KIMBUNGA

I. Kupiga vita suala la uongozi mbaya: Shairi La WENYE NAYO WATUBANA., KIMBWANGAI n.k

II. Kuhamasisha umoja na mshikamano: shairi La KIMBUNGA n.k

III. Kukemea suala La Rushwa katika jamii: Shairi La RUSHWA,

IV. Kuhamasisha kuwajibika katika jamii: Shairi La KAZI, UOKOLEWE n.k

V. Kupiga vita ukoloni mambolea ktk jamii. Shairi La CHUI n.k.

5

MAPENZI BORA:

I. Kuhamasisha jamii kuwa na mapenzi bora: Shairi la ubeti wa 122

II. Kupiga vita suala la chuki katika mapenzi: Shairi ktk ubeti wa 471

III. Kukemea kumfanyia maudhi katika mapenzi: katika ubeti wa 195 - 198

IV. Kupiga vita ubaguzi katika mapenzi katika ubeti wa 126.

Utangulizi:

Aeleze kwa ufupi juu ya mabadiliko chanya. Alama 02.

Kiini

- Hoja nne kila kitabu. Alama 02 @ 16

Hitimisho.

Atoe maoni au mapendekeze juu umuhimu wa mabadiliko chanya. Alama 02.

(Jumla: Alama 20)

6. Swali linamtaka mtahiniwa atumie Riwaya mbili kuelezea suala la mapenzi ya hiari na siyo ya kulazimishwa.

MFADHILI

I. Gaddi Bullah kumpenda Nyambuja

II. Gaddi Bullah kumpenda Dania

III. Bi Hanuna kwa mdogo wake Gaddi Bullah

IV. Dania kumpenda Jerry

V. Gaddi kumpenda Junior

6

# VUTA N'KUVUTE

I. Yasmini kumpenda Denge ingawa ni maskini
II. Bwana Raza kumpenda Yasmini ingawa Yasmini hampendi
III. Bukheti kumpenda Yasmini
IV. Denge kuipenda Nchi yake
V. Mwajuma kumpenda Yasmini na kumpa hifadhi

# USIKU UTAKAPOKWISHA

I. Neli kumpenda chioko ingawa ni maskini
II. Chioko, Neli na Gonza kupendana (wana mapenzi ya kweli)
III. Neli kukataa kutoa Rushwa ya ngono kwa sababu ya mapenzi kwa Chioko
IV. Chioko kuipenda nchi yake kwa kukataa kwenda Zambia
V. Gonza kupenda maisha ya mkato

# KUFIKIRIKA

I. Mtoto wa mfalme kumpenda mwalimu wa kumfundisha.
II. Utubusara ujinga hawa kuipenda kazi ya Ualimu
III. Wananchi wa kufikirika kuipenda nchi yao
IV. Mfalme kuipenda familia yake
V. Mfalme kupenda madaraka.

Zingatia: Mtahiniwa akitaja hoja zingine zisizo hizo apewe alama.

UTANGULIZI
Aeleze kwa ufupi kuhusu dhana ya mapenzi Alama 02
KIINI
Atoe hoja ~~tatu~~ nne (4) kwa kila Riwaya kwa kuonyesha jinsi dhamira za mapenzi zinavyojitokeza kwa namna mbalimbali - (Alama 2×8 = 16)
HITIMISHO
Atoe mawazo juu ya alichokieleza = Alama 02
(Jumla: Alama 20)

7 Swali linamtaka mtahiniwa kuonesha namna watunzi walivyotumia mitindo kufikisha ujumbe kwa jamii katika tamthiliya.

KIVULI KINAISHI

I. Mtindo wa majibizano (Dayolojia)

Mfano: BIBI KIZEE: Watu wakubwa ... (Anang'ona)

Majibizano ya Bi kizee na watoto, tunapata ujumbe kuwa jamii haina budi kuwajali na kuwasikiliza watoto pale wanapo kuwa wanataka kujua jambo fulani.

II. Mtindo wa masimulizi.

Imeoneshwa kupitia mtunzi alivyosimulia matukio mbalimbali ya Giningi kama vile uonevu, dhuluma n.k.

-Tunapata ujumbe Uongozi mbaya husababishwa kuwepo kwa matabaka.

III. Mtindo wa matumizi ya nafsi

Mfano, mwandishi ametumia nafsi zote tatu kama vile nafsi ya tatu umoja pale Wari walipo kuwa wanasema "Aja... Aja... Kumkaribisha Bi-Kirembwe

-Tunapata ujumbe kuwa jamii haina budi kuwapiga vita viongozi wabaya kwani husababisha matatizo.

IV. Mtindo wa matumizi ya tanzu za fasihi simulizi.

-Umeonekana baada ya mwandishi kutumia hadithi iliyosimuliwa na Bi Kizee kwenda kwa watoto kuhusu mambo mabaya ya Giningi.

-Tunapata ujumbe kuwa wazazi na walezi hawana budi kuwasimulia hadithi watoto wao ili kuwajengea ufahamu na uelewa wa mambo.

# MORANI

I. Mtindo wa matumizi ya nafsi
Mfano nafsi ya pili umoja kupitia mazungumzo ya Mlemeta na Nungunungu ambapo tunapata ujumbe kuwa kikulacho ki nguoni mwako.

II. Mtindo wa dayolojia
Imeonekana kupitia mazungumzo ya Mlemeta na Nungunungu alipokuwa akimwambia kuwa jina lako liko kwenye orodha ya wahujumu uchumi.
- Tunapata ujumbe kuwa jamii haina budi kuwa piga vita wasaliti kwani hurudisha nyuma maendeleo.

III. Mtindo wa matangazo
- Imeonekana pale OKASTTA alipokuwa anawatangazia wananchi, wafanya kazi, wakulima na wanafunzi kuwa kutafanyika maandamano.
- Tunapata ujumbe kuwa umoja na mshikamano ni nyenzo muhimu ya mafanikio kwa jamii.

IV. Mtindo wa matumizi ya nyimbo
- Wimbo huu ulikuwa unaimbwa na Malongo ambapo alikuwa anahamasisha kuendelea kupambana dhidi ya wahujumu uchumi
- Tunapata ujumbe kuwa wahujumu uchumi ni watu wanaorudisha nyuma maendeleo.

# NGUZO MAMA

I. Mtindo wa majibizano (Dayolojia)
Mfano: Bwana Sudi na mkewe Bi-pili.

II. Mtindo wa matumizi ya tanzu za fasihi simulizi
Mfano: hadithi hadithi

III. Mtindo wa matumizi ya nyimbo
mfano Nguzo mama, nguzo mama.

7

IV. Mtindo wa matumizi ya nafsi

Zingatia: Mwanafunzi akiandika mtindo aoneshe na ujumbe unaopatikana kupitia mtindo huo.

KWENYE UKINGO WA THIM

I. Mtindo wa majibizano

mfano: LYDIA: Alikuwa aje katika sherehe za hanisi
M2EE: Kifo cha ghafla.

II. Mtindo wa monoloji

mfano: "Ndhisi

III. Mtindo wa matumizi ya nafsi

IV. Mtindo wa kutoa maelekezo

mfano: Elsa Kamata kamata

Zingatia: Mtahiniwa akifafanua mtindo aoneshe na ujumbe unaopatikana kupitia mtindo huo

Utangulizi

Aeleze maana ya mtindo na ujumbe. Alama 02

Kiini

Atoe hoja nne kwa kila tamthiliya, na kwa kila mtindo abainishe ujumbe unaopatikana. (Alama 2 × 8 = 16)

Hitimisho.

Atoe mawazo juu ya alichokieleza: Alama 02

(Jumla: Alama 20)

Swali linamtaka mtahiniwa atumie diwani mbili kueleza jinsi washairi waliweza kutumia jazanda au taswira kufikisha ujumbe kwa jamii, kwa kutoa hoja nne (4) kila diwani.

MAPENZI BORA

(i) Taswira ya Nyamafu inayowakilisha ubaya wa chuki
(ii) Taswira ya Mitume inayowakilisha uzuri wa tabia
(iii) Taswira ya mwangaza inayowakilisha tabia njema kwa watu
(iv) Taswira ya pepo inayowakilisha upepo au furaha.
(v) Taswira ya kileo inayowakilisha ulevi juu ya mapenzi

Zingatia: Na nyingine zisizokuwa hizo mtahiniwa apewe alama.

KIMBUNGA

(i) Taswira ya Kimbunga katika shairi la KIMBUNGA inawakilisha mapinduzi katika uongozi

(ii) Taswira ya nyani katika shairi la KIBWANGAI, inayowakilisha usaliti wa viongozi.
(iii) Taswira ya PUNDA katika shairi la PUNDA inayowakilisha ukosefu wa shukrani
(iv) Taswira ya paka katika shairi la PAKA inayowakilisha tabia mbaya kwa baadhi ya wanaume wenye tabia za kumendea wake za watu
(v) Taswira ya uongozi mbaya katika shairi la VITENDAWILI inayowakilisha viongozi wanashindwa kutekeleza majukumu yao

Zingatia: Na nyingine zisizokuwa hizo mtahiniwa apewe alama.

# FUNGATE YA UHURU

I. Taswira ya Paka shume katika shairi la PAKA SHUME inayowakilisha tabia mbaya za baadhi ya watu wanaopenda kuingilia ndoa za watu.

II. Taswira ya Joka la mdimu katika shairi la JOKA LA MDIMU inayowakilisha kushindwa kwa utawala wakimabavu.

III. Taswira ya mjamzito katika shairi la MJAMZITO inayowakilisha Uongozi mbaya.

IV. Taswira ya bunduki katika shairi la NIKIZIPATA BUNDUKI inayowakilisha madaraka na vyeo

V. Taswira ya sauti katika shairi la NINGEKUWA NA SAUTI inayowakilisha vyeo au madaraka.

# CHUNGU TAMU

(1) Taswira ya mferiji maringo katika shairi la MFEREJI MARINGO, inayowakilisha tamaduni za kizungu kwenye mapenzi

II. Taswira ya daktari na askari katika shairi la DAKTARI ASKARI, inayowakilisha kuponya na kuumiza kwa mtu mmoja

III. Taswira ye mji au sehemu za makazi katika shairi la MANZESE MPAKA OSTABEI inayowakilisha matabaka kati ya matajiri na maskini

IV. Taswira ya ladha mbili tofauti katika shairi la CHUNGU TAMU inayowakilisha shida na raha au uzuri na ubaya

V. Taswira ya maadui wawili katika shairi la CHATU NA KUKU, inayowakilisha maadui wakuu katika jamii

Zingatia: Na nyingine zisizo kuwa hizo mtahini we atitaja apewe alama.

8

UTANGULIZI

Aeleze kwa ufupi kuhusu kazi za asitani (Alama 02.)

KIINI

Atoe hoja nne (4) kwa kila diwani kwa kutaje taswira kisha mashairi na kueleza ujumbe wake. (Alama 2X8=16)

HITIMISHO.

Atoe maelezo, muhtasari au maoni yake juu ya alichokieleza. (Alama 02.)

(Jumla: Alama 20)